

NJOO, UNIFUATE

🦋 Vema, la, hiyo ilikuwa ni kabla ya Becky kuzaliwa. Na kwa hivyo ni—nikawaza, “Vema, unajua . . .” Mimi—mimi hula tu bakuli la unga wa shayiri, unagharimu shilingi kumi. Vema, ninaninii tu . . . Wananipa tikiti yangu, nami ninaitia tu sahihi, mnaona, nami nikailipia, nikairudisha, na kuweka hesabu yake, maana nilikuwa na akaunti ya matumizi.

² Basi siku moja wakati tulipokuwa na mkutano wa—wa wafanya doria. “Jamani,” walisema, “ni nani punguani huyu aliyetoa hesabu ya kitu kama hiki?” Mnaona? Yu—yule kiongozi, mwajua, “Ati senti kumi kwa kiamshakinywa?” Kwa hiyo hicho kinaonekana rahisi sana kwa hao jamaa wengine, mwajua. Wengine wao walitoa hesabu ya dola moja, mnaona; dola mbili kwa chakula cha kutwa. Nami nilitoa hesabu hasa kilichokuwa.

³ Vema, nikasema, “Vema, sasa, hakuna haja ya mimi kutoa hesabu. Ningefanya nini kama nikila tu, senti kumi?”

⁴ Bw. Fields, ambaye alikuwa ni msimamizi msaidizi, akasema, “Billy, weka katika hesabu dola moja, kwa vyovyote vile, angalau.” Kasema, “Hivyo ndivyo hawa wengine wanavyofanya.” Kasema, “Inakupasa kuweka hizo pamoja.”

⁵ “Vema,” nikasema, “mi—mimi sili ila bakuli moja la unga wa shayiri, na hilo ndilo ninalodai.”

Kasema, “Loo, usininii, usifanye hivyo kamwe.”

⁶ Vema, basi nikawaza, “Nitafanya nini nazo?” Basi nikadai senti hamsini kwa kiamshakinywa. Ndipo nikachuka senti arobaini kwake, kama nikitaka kutumia chochote, niwape watoto mtaani; baadhi ya watoto, mwajua, ambao walionekana kana kwamba wanahitaji maskini sambusa ndogo, sambusa, pia. Vema, nilifikiri labda huenda nikaninii . . . Kweli, hiyo ilikuwa ni kampuni, yenyewe, ikiongea nami namna hiyo. Huyu alikuwa ni mtu kutoka kwenye kampuni hiyo.

Kwa hiyo, nikawaza, “Labda nilifanya kosa fulani.”

⁷ Kwa hiyo hapa si muda mrefu uliopita, nikiwa pamoja na mlinda doria . . . Sasa wao hufanya doria na helikopta, mnaona. Kwa hiyo akaja kule na kusimama. Akasema, “Aisee, Ndugu Branham,” kasema, “mti huu unakua.”

Nikasema, “Naam.” Nikasema, “Watoto hucheza chini ya huo huko nje.”

Akasema, “Twaweza kuupogoa?”

Nikasema, “Naam, bali msiukate. Mnaona?”

Akasema, “Vema, tungetaka kuukata. Tutakulipa kwa ajili yake.”

⁸ Nikasema, “La. La. Sitaki muukate.” Vema, ninajua sheria za haki ya kupishana, pia, mwajua, maana niliishughulikia miaka saba. Nikasema, “La.” Nikasema, “Sitaki ukatwe, bali mnaweza kuupogoa.” Nikasema, “Mimi—mimi huupogoa, bali,” nikasema, “mnaweza. Mnaweza kuupogoa mkitaka.” Nikasema, “Mimi, mimi na Ndugu Wood, tunajiandaa kuupogoa. Tunaipogoa hii mingine yote hapa.” Kisha nikasema, “Lakini tungetaka kuuacha huo hapo kwa ajili ya watoto, Joe na hao wengine, mwajua, jamaa wadogo wanaocheza chini ya mti huo.”

⁹ Nikaenda kwenye safari. Niliporudi, ulikuwa umekakwa wote kwa msumeno na kuondolewa. Loo, hayo yangekuwa ni mashtaka ya jinsi gani kwa kampuni hiyo, mnaona, kwa kuukata mti huo, mnaona. Na kwa hiyo nikawaza, “Sasa,” nikasema, “Bwana, hata sitataja hilo.” Mnaona? “Hata kama kuna chochote ambacho mimi—ambacho mimi, juu ya hilo, wakati mwingine nikitoa hesabu, nikila tu cha gharama ya peni moja, na inilazimu kuweka katika hesabu ‘senti hamsini.’” Mnaona? Nikasema, “Kama kuna kitu juu ya hilo, acha hizo ziulipie, mnaona, kwamba—kwamba mimi—kwamba nilipie huo, mnaona. Kwamba mimi...” Ndipo nikaacha kuota kuhusu kuwa katika Shirika la Utumishi wa Umma basi, mnaona, maana hapana shaka ilikuwa ni kitu fulani huko nyuma.

Inatupasa kuangalia tunayofanya. Hatuna budi kukutana nayo siku moja.

¹⁰ Enyi watoto, mkija hapa. Mama yenu alikuwa huku, mwingine leo, Trudy. Nadhani hamkuninii, hamkujua. Hili kidogo linashangaza, naweza kuona. Nanyi mnajiandaa kuhitimu. Nasi tumekuwa na safari hii huku nje pamoja. Nitaenda katika mkutano sasa, mara baada ya mkutano huu. Ndipo tutaenda nyumbani.

¹¹ Nilifikiria ingekuwa ni nafasi nzuri kuwazungumzia ninyi nyote, na halafu pia nikawazia lingekuwa ni jambo zuri kuwazungumzia watoto kidogo tu kabla ya mahafali yenu. Tusome kifungu katika Biblia, ndipo nizungumze nanyi tu kutoka moyoni mwangu, kwa yapata dakika kumi. Nitatoweka niwaondokee. Mnaona?

¹² Kabla sijazungumza na watoto, ningetaka tu kuzungumza na watu wazima kwa dakika moja, pia, ninyi nyote. Sasa ni, labda, huenda imekuwa, safari ngumu. Ila ujuzi ambao nimejifunza kwa Mungu, nisingechukua dola elfu kumi kwa yale niliyojifunza kwa Bwana tangu nimekuwa hapa. Kweli ninaamini nimekuja katika utiifu mkamilifu kwa amri ya Mwenyezi, na ni—ninatumaini ninaweza kubaki namna hiyo daima. Na kuna...

¹³ Nilipokuja, jambo moja, ilikuwa ni kwa ono, kwamba nilikuwa nimesimama juu ya Tucson huku juu wakati m—m—mlipuko ulipotokea. Vema, Ndugu Fred alikuwepo wakati

ulipotokea. Nao wakapiga picha hiyo sasa, mwajua, angani. Na sikuwazia mengi juu yake, kamwe sikuitambua. Kwa hiyo ikaanza kunivutia kwa namna fulani, hivi majuzi. Naye Ndugu Norman, baba ya Norma hapa, akaniambia, kasema, “Uliona hii?”

¹⁴ Ndipo mara nilipoangalia, papo hapo palikuwapo na hao Malaika dhahiri tu walivyoweza kuwa, wamekaa pale pale katika picha hiyo. Mnaona? Nikaangalia nione ilikuwa ni lini, na ilikuwa ni wakati, ule ule, yapata siku moja ama mbili hapo kabla, ama siku moja ama mbili baada ya mimi kuwa kule juu. Nikaangalia mahali ilipokuwa. “Kaskazini-mashariki mwa Flagstaff, ama Prescott, ambao uko chini ya Flagstaff.” Vema, hapo ndipo tulipokuwa hasa, mnaona, papo hapo kabisa.

¹⁵ “Maili ishirini na sita kwenda juu.” Mbona, mvuke hauwezi kwenda zaidi—zaidi ya nne, maili nne, ama tano, unyevu, ukungu wa namna yoyote au chochote kile, mnaona. Ndege huruka kwenye elfu kumi na tisa. Hiyo ni kusudi zipate kuruka juu ya mawingu yote, mnaona. Na elfu kumi na tisa ni kama maili nne kwenda juu. Hii ni maili ishirini na sita kwenda juu, na maili thelathini kuingama, na katika umbo la piramidi, kama umeiangalia hiyo picha.

¹⁶ Na kwenye mkono wa kuume, kama nilivyowaambia, niliona, yule Malaika, amejitokeza wazi kabisa. Huyu hapo, kifua mbele, mabawa nyuma, akiingia moja kwa moja, jinsi tu ilivyokuwa hasa. Sikuiona wakati Wao waliponinii kwanza... Kumekuwako na mambo mengi sana.

¹⁷ Katika tu kushuka nikija barabarani hivi majuzi, kuna jambo lililotokea ambalo lilingizungumzia kuhusu jambo ambalo si—sina budi kufanya. Nao si—si ujumbe wangu.

¹⁸ Wakati mmoja, Leo Mercier alisema, kasema, “Ndugu Branham, wakati utakuja baada ya jambo hili,” kasema, yapata miaka mitano ama sita iliyopita, labda saba, kasema, “Bwana ataibadilisha huduma yako, Ndugu Branham.” Kisha kasema, “Akifanya hilo, labda utapanga tu hospitali, na kuwanena watoke vi—vitandani na kadhalika.” Halikusikika sawa, ingawa ninaamini Ndugu Leo alikuwa akijaribu kuwa mwaminifu kulihusu.

¹⁹ Lakini halikusikika sawa, kwa sababu, mnaona, Bwana wetu Yesu kamwe hakufanya hivyo. Mnaona? Na Yeye alienda katika hospitali. Kulikuwa na mmoja katika hospitali hiyo. Mnakumbuka mahali ilipokuwa katika Biblia? Birika la Bethesda. Umati mkubwa wa watu wasiojiweza ulikaa hapo, viwete, vilema, vipofu, waliopooza, wakimngojea Malaika. Sasa, hiyo ilikuwa katika hospitali ya kiroho ambapo watu waliungojea uponyaji wa Kiungu. Ndipo huyu hapa Mponyaji wa Kiungu Mwenyewe akaingia na kumponya mmoja kisha akaondoka. Kwa hiyo usingetarajia mwanadamu anayepatikana

na mauti, ama huduma ijitokeze, ambayo ingekuwa kubwa kuliko hiyo ilivyokuwa. Mnaona? Nisingekubaliana na hilo.

²⁰ Lakini nilipoanza kugeuka, Roho Mtakatifu akaja juu yangu. Nikamwomba Leo kalamu. Nikachukua kipande cha karatasi, nami nikaliandika. Kiko kwenye trela yake leo hii, iwapo utawahi kuwa mahali ilipo. Ni ile trela ya kale ya alumini ambapo nilikuwa na zana za kupakia mizigo. Unapoingia tu mlangoni, kuna rafu mkono wa kulia, papo hapo mbele ya trela. Kimewekwa hapo chini. Nilikiweka pale juu. Kilisema, “Siku moja mnaweza kukiondoa hiki. ‘Mungu kamwe hataibadilisha huduma, bali Yeye atambadilisha mtu mwenye huduma hiyo.’” Hivyo ndivyo itakavyofanyika.

²¹ Mnaona, ni—ninajua ninalopaswa kufanya, bali si—si—siwezi, siwezi kulifanya katika hali niliyomo sasa. Kwa sababu, inanibidi kuninii...Jambo fulani halina budi kutukia ndani yangu, ambalo lithitaji Mungu kulitekeleza.

²² Tunakusudia kurudi nyumbani. Watoto wanatamani kurudi nyumbani, wote wakitaka kurudi. Kwa hiyo ninawazia kuwarudisha, Bwana akipenda, labda baada ya ibada Jumamosi, na kwa hiyo nirudi. Kutoka hapo, sijui. Ila najua mara hicho kitu fulani kikifanyika ndani yangu, kunifanya nipate hisi ya watu, tofauti na vile nifanyavyo sasa. Nilikuwa nimewakataa wa—watu, mnaona, na mimi—mimi sikutaka kuwa na uhusiano wowote nao tena. Mnajua ninalomaanisha, ninaowaita “riki, riketa,” walikuwa na mambo waliyokuwa wamefanya. Nilihubiri kwa uaminifu wote, naye Mungu alikuwa amelithibitisha kwa kila njia. “Basi ikiwa hawakutaka kuliadini Hilo, mbona, achana nao basi.”

²³ Nilikuwa nikienda kule juu, nikajiunge na Bud msimu huu unaokuja wa kupukutika majani, nianze shughuli kule juu. Ningojee nyikani, niache nywele zangu na ndevu zikue. Ndipo kama Bwana alinitaka kwenda popote, Yeye angenitumia neno, nami ningeshuka kwenda kulitenda.

²⁴ Na nikiwa njiani, nikija hivi majuzi, Yeye alinisimamisha. Nami nikaona mahali ninii...nililokuwa nikijia. Ni—niko njiani mwangu kuendea kitu kingine sasa. Basi nikawazia, nilipofika nyumbani, ningefanya kile tunachoita mazungumzo ya moyo kwa moyo, labda niyaweke kwenye kanda, halafu basi na ili kwamba watu wote wangeona ni kwa nini haya mabadiliko ya ghafla.

²⁵ Sasa, ninyi watoto, hebu tuninii tu...Hebu tuombe kidogo.

²⁶ Bwana Yesu, tunashukuru kwa ajili ya wakati huu, kujua ya kwamba tumekusanyika hapa, vijana kwa wazee, na wenye umri wa makamu. Nasi tumekusanyika, upande huu wa Umilele, mara nyingine tena kuzungumza kukuhusu Wewe na kuhusu mambo yanayohusu Uzima wa milele.

²⁷ Nao hawa watoto wanaoketi hapa usiku wa leo, baadhi yao wanahitimu, wengine tayari wamehitimu. Lakini ninatambua, Bwana, jambo fulani lililotukia saa chache tu kabla ya ule mshindo mkubwa, ama mlipuko mkubwa, lilikuwa limetukia mlimani kule juu, kaskazini mwa Tucson, wakati Malaika wa Bwana walishuka. Ninakumbuka yaliyosemwa, na—na hasa kuhusu vijana. Ninakuomba Wewe, Bwana, utusaidie kuelewa. Basi jalia niweze kusema jambo fulani kwa hawa jamaa wadogo, usiku wa leo, ambalo litawasaidia safarini. Kwa kuwa, Bwana, sote tunahitaji usaidizi huo kwenye wakati huu.

²⁸ Tubariki pamoja. Zisamehe dhambi zetu. Na kama jambo lolote ambalo tumefanya tangu tuwe hapa nje, ambalo halikukufurahisha, tunaomba utusamehe hilo. Kwa kuwa tunatambua, leo hii, ya kwamba hatuna—hatuna hakikisho la kesho. Hatujui kile kesho italeta. Hatuna budi kujiandaa leo kukabiliana na kesho. Pia, Baba Mungu, kuna njia moja tu tunayojua ya kufanya hili, hiyo ni, kujiandaa kukuona Wewe, kwa kuwa baadaye tunatambua ya kwamba sote tutafanya hivyo. Na hatuna budi kukutana nalo wakati mmoja, ama katika amani, kama rafiki ama mtoto, au kama adui. Na iwe mbali, Bwana, kwamba tungekuwa chochote kile ila watoto Wako Mwenyewe wapendwa. Tujalie mambo haya tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

²⁹ Leo hii, nilipokuwa nikifyeka magugu, mapema sana asubuhi ya leo, nilipata mahali katika Biblia, nilipowazia lingekuwa ni jambo zuri kusoma kwenye wakati huu. Na ni . . . huenda pasiwe panapofaa vilivyo, bali niliwazia kwa ajili ya ninii tu. . . ninii tu—dakika chache tu, kuzungumza. Ninataka kusoma hili kutoka kwenye mlango wa 18 wa Luka Mtakatifu. Waandishi wote wanne wa Injili waliandika habari zake. Mlango wa 18 na kifungu cha 18.

Tena, mtu mkubwa mmoja alimwuliza, akisema, Mwalimu mwema, nifanye nini ili nipate kuurithi uzima wa milele?

Yesu akamwambia, Mbona unaniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, naye ndiye Mungu.

Wazijua amri; Usizini, Usiue, Usiibe, Usishuhudie uongo, Waheshimu baba yako na . . . mama.

Tena . . . akasema, Haya yote nimeyatenda, na kuyashika hayo tangu utoto wangu.

Yesu aliposikia hayo alimwambia, Umepungukiwa na neno moja bado; Viuze vyote . . . ulivyo navyo, ukawagawie maskini, . . . nawe utakuwa na hazina mbinguni; . . . njoo, unifuata.

³⁰ Nafikiri, neno Njoo, Unifuata, huo ndio ushauri mzuri kuliko wote ningeweza kutoa kama nilikuwa nikizungumza na watoto elfu kumi, ama kama nilikuwa nikizungumzia tu wale

ninaowazungumzia. Ni amri, na jambo lililo kuu zaidi ya yote ambalo nafikiri liliwahi kutolewa kwa mtu yeyote, na hasa sana kijana, “Nifuata.”

³¹ Itakubidi kumfuata mtu fulani. Sasa, unaninii tu... Unaweza kukumbuka hilo. Itakubidi kumfuata mtu fulani. Na jinsi unavyomfuata mtu huyo, kuwa na hakika ya kwamba, mtu huyu anamfuata nani. Unaona? Sisi...

³² Paulo wakati mmoja alisema, “Iweni wafuasi wangu kama vile mimi nilivyo wa Kristo.” Kwa maneno mengine, “Kama tu ninavyomfuata Kristo, ninyi nifuatani.”

³³ Na sasa, kwenye kipindi hiki cha badiliko, hiki—hiki kipindi cha maisha ambacho sote tutafikia. Na mara nyingi mmenisikia nikipiga makelele, “riki, riketa,” na kadhalika. Ni, ni wakati. Ni wakati tunaishi. Hakika si hao watu.

³⁴ Hao watu ni watu kama tulivyo sisi. Hao watoto huko nje wakiwa na magari haya yanayoenda kasi sana, wakiendesha mbio huku na huku barabarani, na kufanya vituko jinsi wanavyofanya, wakivuta sigara na kunywa pombe, na wasichana wamevaa kizinifu, na kadhalika, hao ni wasichana na wavulana kama tulivyo sisi. Mnaona? Hao ni wanadamu. Wanapenda. Wanakula. Wanakunywa. Wanalala. Wanapumua. Hawana budi kufa. Hao ni watu kama tu tulivyo sisi. Nao hata hivyo wamekuwa...

³⁵ Wamepagawa na roho mchafu. Hawajui hilo. Sio kwa sababu ya—ya hao watu, bali ni kwa sababu, wakati mwingine, kiongozi fulani ambaye wamekuwa wakimfuata amewaongoza kwenye barabara mbaya.

³⁶ Sasa, ninyi wasichana na wavulana mnajua vizuri kuliko hivyo. Mnajua. Mmefundishwa vizuri kuliko hivyo. Mna wazazi bora zaidi, mafunzo bora zaidi kuliko kufanya jambo kama hilo. Mnajua vizuri zaidi.

³⁷ Lakini hao hawajui, mnaona, kwa sababu makanisa wanayohudhuria ni makanisa ya kisasa, mamboleo. Na wao—wao wanaishi tu kwa ajili ya siku, kupendwa sana na watu. Na, loo, jamani! Ni nini... Uadilifu unakuwa ni wema kwao. Mnaona? Kwa hiyo wao, kile... Kama nilivyosema wakati mmoja, katika mchezo nilioona hapa chini, sio muda mrefu uliopita, wa Sodoma na Gomora, kwamba mwanamke huyu aliyepagawa na pepo mchafu alimwambia Lu—Lutu, “Unachoita utovu wa uadilifu, ninakiita wema.”

³⁸ Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Kwa hiyo tumerudi mahali hapo tena.

³⁹ Hebu tumwangalie jamaa huyu, kwa dakika chache, tuliyesoma habari zake. Hapana shaka kwamba mtoto huyu alizaliwa katika nyumba nzuri, kama ninyi watoto mlivyojaliwa.

Alilelewa na wazazi wazuri. Maana, ilithibitika, wakati Yesu alipomwonyesha zile amri za Mungu. Yeye alisema, “Nimezishika hizi tangu utotoni.” Ilionyesha ya kwamba alikuwa—alikuwa—alikuwa amelelewa vizuri. Yeye hakuwa tu mtukutu. Nanyi mwajua, a—alikuwa amelelewa kujua yaliyo mema, watoto kama mlivyo ninyi nyote. Labda alikulia chini ya mama na baba wacha Mungu, ku—ku—kumfundisha mema, alipokuwa mtoto. Vema, hilo ni jema.

⁴⁰ Labda, kama mtoto mchanga, mama yake alikuwa na malengo makuu ya yeye kuwa mtu mashuhuri siku moja. Baba yake alikuwa ni tajiri, ambaye angeweza kumsomesha na—na kumpa elimu aliyoweza... angetokea na elimu nzuri na kuweza kuwa kitu fulani ulimwenguni. Na kwa uaminifu wa mama huyu na baba, kumwelimisha mtoto huyu, na labda kufikia wakati wake wa mahafali kama vile mmefikia, mnaona, wakati alipopitia shuleni na akapata elimu yake. Hapana shaka kwamba labda alikuwa ndiye fahari na furaha ya—ya maisha ya mama na baba. Hapana shaka, katika siku hizo, alikuwa na farasi wazuri, kama vile mlivyo na motokaa, na baba mzuri na mama kama vile ninyi nyote mlivyo nao, wanaohakikisha, mna nguo nzuri, na—na motokaa, na mnaweza... na kufurahia tu maisha, kitu tu kama mliche nacho siku hizi.

⁴¹ Nao baba na mama wakiwa na... wakiomba siku zote kwamba—kwamba mwanao asingegeuka kuwa mtu wa kawaida tu, kwamba angekuwa mtu asiye wa kawaida. Wazazi wote wanataka hilo. Mlimsikia Yesu akirejea kwenye amri hiyo, “Waheshimu baba na mama yako,” kisha akakoma? Mnaona? Na hilo ndilo lengo la mzazi yeyote, kufanya mazuri wawezayo, kwa watoto wao, wawaelimishe, wawape vitu ambavyo labda wao hawakuweza kuvipata. Hivyo ndivyo ninavyojisikia kuhusu watoto wangu.

⁴² Nafikiri, wakati mwingine, katika kwenda shuleni, sasa; Nafikiri, ati niwapeleke Becky na Sarah na Joseph kwenye sekondari hizi za juu na kadhalika, ambako haya yote yanaendelea? Nafikiri nitawachukua na kuenda huko nyuma mlimani, na—na kuwalelea kule juu pamoja na... kama Wahindi wanavyoishi.

⁴³ Lakini jambo ndilo hili. Kile kilicho ndani ya mtoto kitajitokeza. Haidhuru iwe ni wapi, hakina budi, kitajitokeza. Kama ni uovu humo ndani, utatokea kwenye kambi ya Kihindi. Kama ni mema humo ndani, yatatokea kwenye kambi yoyote. Mnaona? Ni kile kilicho ndani ya mtoto huyo, tabia ya mtoto huyo, kile kilicho ndani yako. Na kile ulicho sasa ndicho labda utakachokuwa maishani mwako mwote. Uko katika mahali pa kubadilikia.

⁴⁴ Mnajua nini? Asilimia themanini na sita ya wongofu kwa Yesu Kristo hufanyika kabla ya umri wa miaka ishirini na moja.

Zinaonyesha. Takwimu zinaonyesha hilo. Asilimia themanini na sita wamjiao Kristo, humjia kabla hawajafikia umri wa miaka ishirini na moja. Wewe, ukiisha kupita umri huo, unaumbika zaidi ama kukakamaa katika njia zako. Loo, inawezekana, hakika. Wanakuja, umri wa miaka sabini, themanini, bali ni kwa nadra sana. Unaona?

⁴⁵ Unajiumba wakati ukiwa kijana. Unaelekeza malengo yako kwa yale unayotaka kufanya, na yale unayotaribu kufanikisha maishani. Unayawazia. Na unapowazia, hakika, nia yako, hilo linawasilishwa niani mwako na kitu fulani kisichojulikana ambacho—ambacho huitawala nia yako. Ndipo basi wakati linapoingia niani mwako, basi unalinena, kwamba utalitekeleza. Halafu basi malengo yako yanakusukuma kwake.

⁴⁶ Kwa hiyo, mama na baba, wakimtarajia kijana huyu kuninii. . . malengo yake ya kuwa mashuhuri; pesa za kutosha kuzitekeleza. Halafu basi, hapana shaka, waliomba ya kwamba m—mvulana huyu mdogo ange—angeipata nafasi hiyo. Unaona, wa—walikuwa wamefanya yote waliyoweza. Huenda ana farasi wazuri, na—na labda alikuwa anapendwa sana miongoni mwa wanawake.

⁴⁷ Na kile ambacho kingempendeza mwanamume, kingempendeza mwanamke, na vinginevyo, mnaona, maana tunazungumza juu ya maisha ya binadamu, nafsi, wanaume na wanawake pia.

⁴⁸ Halafu basi, baada ya nafasi hii yote aliyokuwa nayo mvulana huyo, mnaona, aliingia kwenye “hali ya utajiri,” tunavyosema, mahali ambapo haikumbidi kuhofia mengi kupita kiasi. Wazazi wake walikuwa na pesa. Alikuwa na. . . Yeye alikuwa ninii sana. . . Akawa mtawala. Biblia inarejea hilo hapa, wa ninii. . . kama kijana tajiri, mtawala. Nasi tunaona ninii. . . Kwenye umri mdogo, labda katika utineja wake, ndio kwanza tu atoke shuleni, ndio kwanza atoke kwenye mahafali, labda, majuma machache hapo kabla, ama kitu fulani, akawa. . . Yeye ni mtawala, naye alikuwa na yote ambayo mioyo ingeweza kutamani.

⁴⁹ Wala mvulana huyo hakuwa riki mamboleo. Yeye ni mtoto mzuri. Ninaamini, wakati Luka alipoandika habari zake, ama Marko, ninaamini ndiye, Yesu alimwangalia akavuta pumzi, kwa sababu alimpenda. Mnaona? Kuna jambo fulani kuhusu mtoto huyo. Kulikuwako na haiba nzuri iliyoambatanishwa na mtoto huyu. Alitoka wapi? Kutoka kwa familia nzuri iliyokuwa imemfundisha amri za Mungu, na kuhakikisha ya kwamba alizishika. Naye alizishika, tangu utoto wake na kuendelea.

⁵⁰ Basi mvulana huyu alikuwa na lengo; alitaka Uzima wa Milele. Akasema, “Mwalimu Mwema, ningeweza kufanya nini kuurithi Uzima wa Milele?”

⁵¹ Unaona, kwa yote uliyo nayo ulimwenguni, hata hivyo nafsi iliyo ndani yako inakwambia kuna kitu unachohitaji, ambacho huna. Kwa utajiri tu. . . Ama, si lazima sikuzote iwe ni utajiri. Inaweza kuwa, umaarufu, msichana mrembo, ana urembo wake anaoweza kuuwazia. Labda yeye ni maarufu sana shuleni. Labda mvulana anaweza kumpata msichana yeyote atakaye. Anajisikia ya kwamba kwa namna fulani yeye ni salama. Huo sio usalama. Huo utatoweka tu kama ua uwandani. Mnaona? Utapotea. Hautachukua muda mrefu. Mizunguko michache tu ya jua, huo umetoweka, ndipo una nafsi ambayo haina budi kuishi Milele.

⁵² Naye mtoto huyu mdogo hapana shaka alikuwa na haiba nzuri, kwa sababu alijikabidhi kwa Bwana Yesu, akijua aliinamisha goti lake. Akasema, “Mwalimu Mwema, ningeweza kufanya nini niupate Uzima wa Milele?”

⁵³ Yeye akasema, “Mbona unaniita mwema,” kasema, “wakati ukijua kuna Mmoja tu aliye mwema, na huyo ni Mungu?” Mnaona? Kijana huyo alieleza nini katika hili? Ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu. Mnaona? Akasema, “Wazijua amri. Zishike.”

Kasema, kwa hiyo akasema, “Amri zipi, Mwalimu?”

⁵⁴ Yeye akasema, “Zile amri za ‘waheshimu baba yako na mama yako,’ na kadhalika.”

⁵⁵ Akasema, “Haya nimefanya, tangu utoto wangu kuendelea. Unaona, nimezishika hizi.”

⁵⁶ Akasema, “Hata hivyo umepungukiwa neno moja. Nenda, kauze ulivyo navyo, ukawagawie maskini, kisha unifuate.”

⁵⁷ Ni nafasi ya jinsi gani! Huyu angeweza kuwa ni Petro, Yakobo, ama Yohana, mmoja wao. Mnaona, mtoto huyo alikuwa amefunzwa na kulelewa vizuri, naye alikuwa amepelekwa kwa Kristo, apate kumtumia katika vipaji vyote alivyokuwa navyo ndani yake, kutumia, labda mwenye elimu, kijana, tajiri, mwenye ushawishi, ambako angeweza kuipeleka Injili, na hata hivyo akaikataa. Hilo lilikuwa ni ja—jambo la kijinga jinsi gani kwa mvulana huyo mdogo! Mnaona?

⁵⁸ “Unifuate.” Sasa, mnaona, ilimbidi kufuata mtu fulani. Sasa, alikuwa ama aufuate ushawishi wa watu aliohusiana nao, ushawishi wa msichana fulani, ushawishi wa kundi fulani la wavulana aliokuwa anashiriki nao, wenzake shuleni, ama amfuate Yesu Kristo. Katika wema wake wote, hata hivyo alijua hakuwa na Uzima wa Milele.

Enyi watoto, hilo ndilo mnalopaswa kuwazia. Mnaona?

⁵⁹ Sasa mwangalie mvulana huyo usiku wa leo, kile angaliweza kuwa, na kile alichu, kile alichu usiku wa leo. Yeye yuko mahali fulani. Alikuwa ni mwanadamu. Yuko mahali fulani. Anaingojea Hukumu. Anangojea kuikabili Hukumu kwenye Siku ile, kuikataa nafasi ile ile inayotolewa kwenu enyi watoto, karibu chini ya hali ile ile ya mambo; watoto wazuri, haiba

nzuri, baba na mama wazuri, vile mlivyo navyo, hata hamuhitaji kufanya kazi 'sipokuwa mwe mnataka. Mnaona?

⁶⁰ Bali kuna kitu kingine kinachoambatana na hayo. Kuna jambo fulani ambalo huambatana na hayo. Hilo Neno, usiku wa leo, halifi kamwe. Lingali ni changamoto kwa kila kijana mwanamume, kila kijana mwanamke, "Unifuate." Mnaona?

⁶¹ Maneno hayafi. Wakati wowote unaposema chochote, kumbuka tu, kama ni kwenye gari lako ama katika siri, kama ni mimbarani, kama ni huko chini pembeni mwa barabara pamoja na rafiki yako mvulana ama rafiki msichana, popote pale, kamwe hayafi. Ha—hayana budi kuishi milele.

⁶² Wakati nilipomwona yule msichana ambaye mimi... hivi majuzi usiku katika ono, msichana mdogo mrembo, mchezaji wa Hollywood, nami nikamwona akifa, akifikia, akijaribu kupata usaidizi. Alikufa kwa mshtuko wa moyo, Binti Monroe. Halafu hiyo imekuwa miaka miwili iliyopita, nami nilimwona akifa. Ndipo siku mbili baadaye akafa.

⁶³ Halafu, hivi majuzi usiku, nilisikia sauti ya msichana huyo. Vipi? Watoto walikuwa wakiniambia, "Baba, wewe huenda huko kwenye ule Mto Wa Kutokurudi, wakati wote." Kasema, "Wana mchezo kama huo unaokuja, usiku wa leo." Wakaniambia usiku fulani utakapokuwako, juma moja ama mbili kabla ya wakati. Nikawaza, "Vema, ninataka kuiona hiyo, maana nimekuwa chini kwenye mto huo, mara mbili ama tatu; karibu mara tano, nafikiri." Vema, ni—nilitaka kuuona.

⁶⁴ Naye Binti Marilyn Monroe aliucheza huo. Vema, huyo alikuwa ndiye msichana niliyemwona katika ono. Basi alikuwa ndiye huyo hapo, katika picha, na yale matendo, tendo lenyewe alilofanya kwenye *Mto Wa Kutokurudi*, wakati alipopiga picha hiyo, labda miaka kumi na mitano iliyopita. Ilikuwa ni picha ya kale, labda miaka ishirini iliyopita. Naye amekuwa amekufa miaka miwili. Naye yule pale tena, yu hai, kila tendo na kila neno. Mnaona? Lingali limeshikwa katika kanda ya sumaku hata ni hai tena.

⁶⁵ Isitoshe, bali kila kitu tunachosema ni hai. Kila neno tunalonena haliwezi kufa. Maneno sasa yanapitia kwenye chumba hiki, viwiliwili vya watu. Televisheni huvinasa. Unaweza kunena papa hapa, nao watakusikia kote ulimwenguni, sekunde hiyo hiyo. Hata kabla hujaweza kuisikia katika chumba hiki, inaenda kote ulimwenguni, kwa elektroniki.

⁶⁶ Nayo skrini kubwa ya Mungu inayanasa hayo. Na kila hatua na kila tendo unalofanya, huna budi kukutana nalo kwenye Hukumu. Unaona? Kwa hiyo, ewe jamaa mdogo, ni jambo zuri kusimama, kuwazia juu ya mambo haya, unaona, maana utakutana nayo tena. Unaona?

⁶⁷ Hebu tumfuatilie kijana mwanamume huyu, nafasi aliyokuwa nayo, na ujiweke mahali pake. Na msichana, kama tu ilivyo kwa Becky na Marilyn, kama vile tu kama ulikuwa umesimama mahali pake, na ungeweza kusikia Sauti hiyo ambayo ingali hai.

⁶⁸ Ingali hai. Ingali inatembea. Sayansi inasema, “Katika miaka ishirini tangu sasa, watainasa Sauti Yake halisi aliyonena, miaka elfu mbili iliyopita.” Ingali hai. Kama vile changarawe ikianguka baharini, mawimbi hayakomi. Yanaelekea ufukoni, maelfu ya maili, kisha yanarudi.

⁶⁹ Sauti ikiisha kunena hewani namna hiyo, haifi kamwe. Hakuna kitu unachoweza kusema Hukumuni. Iko pale pale. Kutakuwako na Sauti ya Yesu Kristo ikimsihi yule kijana mwanamume, “Unifuate,” naye akikataa, kwenye skrini, amekunja uso, kwa sababu alikuwa na mali nyingi. Mnaona? Huenda hata tusiwe... Sio sikuzote iwe ni pesa. Inaweza ikawa ni vitu vingine. Unaona? Chochote tunachopenda zaidi ya tunavyoupenda huo wito, unaona, kinakuwa kama ni pesa kwetu. Kinakuwa kitu kinachotupotosha.

⁷⁰ Sasa hebu tumfuate kidogo. Ni kitu gani kinafanyika anapogeuka na kuondoka? Hakuisikiliza hiyo Sauti ya Kristo. Alienda pamoja na marafiki zake.

⁷¹ Ambalo, ninyi watoto, nyote ni watoto wazuri, nanyi hamna budi kuwa na marafiki, lakini angalieni ni rafiki wa aina gani uliye naye. Kama rafiki huyo anamfuata Kristo, ambatana na rafiki huyo. Mfuate Kristo, pia. Lakini asipomfuata, usiambatane naye.

⁷² Hebu na tumtazame. Tunaona, labda alidumisha marafiki zake. Akawa mtawala mkuu. Alikuwa ni mtawala wakati huo. Baadaye, tunamwona amefanikiwa sana mpaka i-i-ilimbidi kujenga maghala mengine kuweka vitu vyake ndani. Ndipo basi akajiambia, akiisha kuzeeka, na shughuli za maisha ya ujana na kadhalika zimepita, yote aliyofanya, labda, yalikuwa burudani.

⁷³ Wakati mwanamume mzee ama mwanamke mkongwe, kama mimi, mke wangu, mama zenu na baba, karibu hawana chochote wanachoweza kuwazia. Hawawezi, hawataki kutoka nje na—na kukimbia huku na huku mitaani, mwajua, kama—kama jamaa wadogo wangepanya, na wasichana. Miadi, na ni nani atakayekuwa mke wako ama mume wako, ama, unaona, hawana hayo niani mwao. Wao, wana watoto, wanavutiwa. Hiyo itakuwa ni ninyi nyote, kesho, kama kuna kesho. Mnaona?

⁷⁴ Hebu mwangalieni jamaa huyu, basi, akiwa labda na... Labda hata hakua. Na, hata hivyo, alikuwa ni mtawala mkuu. Naye aliketi kwenye...

⁷⁵ Basi kama vile ilivyo Yerusalemu, bado, leo hii, wao hula juu darini, wakati huu wa siku, inapokuwa baridi, huko nje jioni.

Ndipo tunaona mtu mwingine ameonyeshwa pamoja naye: ombaomba.

⁷⁶ Naye mtu huyo, kutokana na kulelewa kwake ku—kumheshimu jirani, na kuwatendea wengine kama vile ungetenda wengine wakutendee. Mnaona, kwa kuukataa wito huo wa Kristo, hatimaye. . . Inaonekana kana kwamba, mvulana aliyekuwa amelelewa katika nyumba kama hiyo kwamba, hilo lisingeweza kumwacha, bali lilimwacha. Lilimwacha.

⁷⁷ Basi yule pale mtu amelala langoni, jina lake Lazaro, akimwomba chakula, bila mafanikio. Angelikula makombo aliyoyafagilia mbali, si hata kwa huyo ombaomba, bali kwa mbwa. Naye alikuwa na vidonda vingi. Lakini mtu huyo alikuwa amestaarabika sana katika jamii, wakati huo, hakuwa na hisi tena. Akawa ganzi, kwa sababu alikuwa amekataa ule wito wa Kristo.

⁷⁸ Ndipo labda jioni moja, wakati huu, akitoa pongezi yake kwa divai nzuri, na wanawake wa kupendeza, waliopambwa vito, wamemzunguka, na vitu kama hivyo, pamoja na yote mioyo yake ingetamani, akitoa pongezi kwa kinywaji. Ombaomba amelala langoni.

⁷⁹ Na kabla machweo hayajapambazuka, kesho yake asubuhi, alikuwa kuzimuni, akimlilia huyo Lazaro aje aweke maji kwenye ulimi wake. Badiliko la mandhari.

⁸⁰ Nanyi mnaona, wakati aliposema, “Baba Ibrahimu,” sasa, angali alikumbuka ya kwamba Ibrahimu alikuwa ni baba wa Wayahudi. Akasema, “Baba Ibrahimu, mtume ombaomba huyo Lazaro ashuke aje hapa na maji kidogo vidoleni mwake, ayaweke midomoni mwangu. Miali hii inanitesa.”

⁸¹ Kisha akasema. . . naye Ibrahimu akasema, “Ni, siwezi kufanya hivyo,” kwa kifupi. “Na licha ya haya yote, unaona, ulikuwa na nafasi yako maishani.”

⁸² Alikuwa nayo lini? Hapo Yesu aliposema, “Unifuata.” Lakini akaikataa. Alipitia njia ambayo angeweza kupata pesa. Na hilo ni sawa, hakuna ubaya wa kutafuta pesa, ila umfuata Yesu wakati ukifanya hivyo. Unaona? Naye alikuwa amepitia njia nyingine, pamoja na umati.

⁸³ Nanyi mnaona, yeye alisema, naye Ibrahimu alisema, “Tena zaidi ya haya yote, kuna shimo lililowekwa kati yako na yeye, ambalo hakuna mtu aliyewahi kuvuka, wala kamwe hataweza. Wale walioko kule hawawezi kuja hapa, na hawa hapa hawawezi kwenda kule. Limewekwa. Hakuna mtu aliyewahi kuvuka au atakayelivuka.”

⁸⁴ Basi msikilizeni. Yeye anataka kuwa mwinjilisti basi. Ule wito ambao Yesu alikuwa amempa, ku—kumfuata Yeye, ulikuwa, na kuwavuta watu, kama kijana mwanamume, ulimrudia tena.

Akaukumbuka, kwamba alikuwa na ndugu watano, na huko nyuma duniani, na hakutaka wawe mahali hapo.

⁸⁵ Akasema, “Mtume Lazaro, basi, arudi huko akawaambie ndugu zangu wasije huku.” Kwa maneno mengine, “Wakubali wito wa, ‘Unifute.’” Mnaona?

Lakini akasema, “Hao, hawatakubali.”

⁸⁶ Akasema, “Naam, kama mtu angefufuka kutoka kwa wafu, kama vile Lazaro, na kurudi akawaambie.”

⁸⁷ Mnaona, inaonyesha ya kwamba, tukiisha kufa, ungali na fahamu zako. Alikumbuka. Ibrahimu akasema, “Mwanangu, kumbuka, katika siku zako.” Unaona? Ungali unakumbuka. Hupotezi kumbukumbu yako. Unakumbuka.

⁸⁸ Na kumbukumbu ambazo mtu anaweza kuwa nazo, na angali mahali pale pale, alikumbuka nafasi aliyokuwa nayo ya kumsikiliza Yesu akisema, “Unifuate.” Lakini yeye alimfuata mtu mbaya, umati mbaya. Aliingia katika umati mbaya, na kuenda mahali pabaya, akaishia kwenye Umilele mbaya; ataangamizwa kwenye Siku hiyo, kutoka kwa Mungu milele.

⁸⁹ Yesu pia alisema neno kuu la kushangaza, “Hata mtu akifufuka kutoka kwa wafu na kurudi, hata hivyo hawatashawishika. Maana, wanayo torati ya Musa, na ikiwa hawataisikia hiyo, basi hawatasikia hata mtu akifufuka kutoka kwa wafu. Hawatahawishika.”

⁹⁰ Kwa nini? Kwa nini? Je, torati ilisema jambo kama hilo? Ndiyo. “Watendee wengine jinsi ungetaka wakutendee.” Naye alikuwa ameishi chini ya sheria hiyo. Lakini alimwacha yule mwombaji afe langoni. Mnaona? Yeye alikuwa—alikuwa ameishi chini ya amri za Mungu, na hata hivyo akashindwa kuuona ule Uzima mkuu wa Milele.

⁹¹ Enyi watoto, ninyi, kila mmoja, mnaonekana kama wangu. Ninyi, kila mmoja, mnaonekana kama tu wana na binti zangu. Kwa njia moja, ndivyo mlivyo, mnaona, tukinena kiroho. Hiyo ni kweli. Bwana Mungu ame—ameziweka nafsi zenu katika ulinzi wangu, kwa sababu mnakuja, kunisikiliza. Mnaniamini mimi. Mnaona? Na katika maana moja ya neno hilo, ninyi ni wana na binti zangu. Hiyo ni kweli.

⁹² Daima kumbukeni, kuzishika amri za Mungu ni jambo kuu. Kulelewa katika nyumba nzuri ni urithi kutoka kwa Mungu. Na kuwa watoto wazuri wenye haiba kama mlivyo nazo, vema. Vizuri sana, kuwa na elimu. Ni vizuri sana hata kuishi katika nchi hii huru. Tuna mambo mengi ya kutolea shukrani.

⁹³ Ila kuna kitu kimoja ambacho hukirithi. Inakubidi kukikubali. Hicho ni Uzima wa Milele. Nawe utafanya hivyo tu kwa kumfuata Yesu, kwa ujuzi wa kuzaliwa mara ya pili. Usipuuzie hilo.

94 Hadithi ndogo niliyosikia wakati mmoja, ya mtu ambaye alikuwa, loo, alikuwa maskini. Na sikuzote a—alitaka kuninii . . . Ni hadithi ndogo ya vichimbakazi, yaonekana. Daima imedumu pamoja nami, hata hivyo. Basi siku moja aliokota ua. Nalo hilo ua lilikuwa ni la kiajabu, na ua likamjibu, likasema, “Umekuwa maskini maisha yako yote.” Akasema, “Sasa omba utakalo, nawe utapewa.”

95 Akasema, “Kwamba mlima huko ng’ambo utafunguka, nami ningeweza kuingia mle ndani na kupata dhahabu mlimani.”

96 “Vema,” akasema, “itakubidi kunichukua mimi kwenda pamoja nawe popote uendapo. Unaona? Itakubidi kunichukua mimi twende pamoja nawe. Kwa hiyo, popote nilipo, basi unaweza kuomba utakalo.”

97 Akaenda mlimani, ndipo mlima ukafunguka, akaingia. Rafu zilikuwa zimejaa dhahabu na almasi, kama vile maskini hadithi hiyo ya vichimbakazi inavyoenda. Akaliweka lile ua chini juu ya—juu ya meza, ama, mwamba. Kisha akakimbia akanyakua kito kikubwa mno, na akasema, “Lazima niende niwaonyeshe hiki marafiki zangu. Na sasa mimi ni tajiri. Nina kila kitu sasa. Sina budi kuonyesha hiki.”

98 Na kwa hiyo lile ua likanena, “Lakini,” likasema, “umesahau kitu muhimu.”

99 Kwa hiyo akarudi nyuma mbio na kuokota, kasema, “Vema, labda nita—nitachukua kipande cha dhahabu. Nitachukua kipande cha fedha.” Na kwa hiyo akasema, “Nita—nitaharakisha nitoke, nikawaambie watu jinsi nilivyo tajiri, na yote niliyo nayo.”

100 Basi akafika mlangoni, nalo ua likasema, “Lakini umesahau kitu muhimu.”

101 Kwa hiyo anarudi mbio tena. Akasema, “Humu ndani tunapata kila namna ya nyenzo.” Kwa hiyo, akaokota jiwe. Akasema, “Nitaenda, nichukue jiwe hili nikawaonyeshe watu mlima huu umefanyizwa kwa jiwe la aina gani, ili kwamba niweze kupata njia yangu ya kuurudia.” Mnaona?

102 Basi akaanza kutoka mlangoni, nalo lile ua likasema, kwa ninii . . . mara yake ya mwisho, “Umesahau kitu muhimu.”

“Loo,” akasema, “loo, nyamaza.”

103 Mnaona, hakutaka kuisikia tena, “Ulisahau kitu muhimu,” ndipo akatoka mbio mlangoni. Basi alipofanya hivyo, mlango ukafungwa nyuma yake, huku lile ua likiwa ndani. Kitu muhimu kilikuwa ni lile ua. Mnaona? Kitu muhimu kilikuwa ni lile ua.

104 Miaka kadhaa iliyopita, kama mtoto mdogo, jinsi mlivyo nyote, hapa, ranchi ya ng’ombe hapa juu, juu ya Phoenix. Nilikuwa nikisoma kijikaratasi, juu ya kutafuta madini, gazeti kuhusu mtafuta madini. Wakati huo, hakukuwako na barabara

kupitia hapa basi, vijia tu vya mchanga. Wangali wanafanya utafutaji mwingi wa madini hapa ndani, mwajua.

¹⁰⁵ Lakini mtafuta madini huyu alikuwa ameingia, naye alikuwa amepata pesa nyingi sana, na kupata dhahabu nyingi. Basi alipokuwa akiingia, alikaa kwenye kibanda alichokuwa amepata. Naye alikuwa na mbwa, na, hu—huyo mbwa, amefungiwa hapo nje. Ndipo usiku huo, kulikuwako na haramia aliyekuwa akimvizia, akamnyang'anye dhahabu hii. Aliichukua kutoka kwenye mashimo ya kale ya Kihispaniola, naye alikuwa akija nayo. Ndipo mbwa akaanza kubweka.

¹⁰⁶ Na mtu huyo hakutaka kusumbuliwa na mbwa huyo. Akasema, “Nyamaza.” Akasema, “Kesho, nitaipeleka hii ndani, m—mjini.” Nami nitaninii. . . Mafundisho ya hadithi hii yalikuwa ni haya. “Nami nitaipimisha, ndipo nitakuwa tajiri. Nami nitanunua magari makubwa. Na nitakuwa na wanawake wa kila namna na karamu nyingi kubwa. Nami nitakuwa tajiri, kwa sababu tayari nimeshaweka madai ya umilikaji. Ninayo dhahabu hapa, nyingi.” Kisha kasema, “Nitaninii. . .”

¹⁰⁷ Ndipo wakati alipokuwa akijaribu kupata usingizi, yule mbwa akaendelea kubweka, kwa sababu mbwa alimwona huyo haramia akija, akinyemelea, akingojea mtafuta madini alale.

¹⁰⁸ Akaamka tena, na kumpigia mbwa makelele tena, kasema, “Nyamaza.” Ndipo maskini mbwa yule akalalama kwa woga na kujaribu kumwonya bwana wake kwamba hatari ilikuwa ikivizia—ikivizia. Ndipo wakati aliponinii. . .

¹⁰⁹ Mara nyingine, wakati mbwa alipoanza kubweka, huyo mtafuta madini alikuwa na bunduki ya marisau. Hakutaka kusumbuliwa, kwa hiyo alisimama tu na kumpiga mbwa risasi. Basi huyo mtafuta madini akauawa usiku huo, na yule haramia. Ndoto zake zote za ajabuajabu hazikumsaidia. Kwa nini? Aliinyamazisha sauti iliyokuwa ikimwonya.

¹¹⁰ Hakuna mtu anayeweza kujaribu kufanya lolote, enyi watoto, angeweza kamwe kufanya lolote baya, baada ya kulelewa jinsi mliyovolelewa, isipokuwa utajisikia kitu fulani kikikwambia usilifanye. Sasa, kamwe usiinyamzishe sauti hiyo inayokuonya.

¹¹¹ Pia daima kumbuka, ikubali Sauti hiyo iliyosema, “Unifuate,” na daima utatokea vizuri. Ninaamini utatokea. Nina matumaini nawe. Lakini sikuzote kumbukeni ya kwamba Yesu, hiyo Sauti, iko hai duniani usiku wa leo.

¹¹² Ni sawa tu, kama kila sauti na kila neno tulilonena bado lipo hai, wakati hiyo sauti inapotoka ikaenda pamoja na hilo wimbi la peponi la hewa. Ninii. . . Mnaona, una mtambo hapa wa kuipeleka nje. Wewe ndiwe ule mtambo wa kurusha nje. Sasa inahitaji kituo fulani kuinasa.

¹¹³ Na Yesu alikuwa ndiye Mtambo wa kurusha Neno la Mungu, kwa kuwa Yeye alikuwa ni u—utatu wa Mungu ukidhihirishwa katika Mtu mmoja. Alikuwa ni Mungu mkamilifu na Mwanadamu mkamilifu.

¹¹⁴ Nao utatu wa Mungu, utatu wa sifa za Mungu, kuwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, uliwakilishwa katika Mtu huyo mmoja, Yesu Kristo. Kwa hiyo, pale, Yeye alikuwa ni Neno.

¹¹⁵ Na Yeye alikuwa ndiye ule Mtambo uliosema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Mnaona? “Amin nawaambia, yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele.” Sasa, Neno hilo limetoka kwenye Mtambo wa kurushia. Yeye alisema, siku moja, “Amin nawaambia, ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ na usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale uliyosema yatatimia, yatakuwa yako.”

¹¹⁶ Sasa, laiti ungalikuwa tu ndiye kituo cha kunasa Hilo, kwa udhibiti fulani ndani yako, kwa imani, itakuvingiza moja kwa moja katika duara ya Mungu, kwenye Kuzaliwa upya, na kuzaliwa mara ya pili. Ndipo sikuzote utakuwa na mawasiano, kuisikia Sauti hiyo ambayo sikuzote itakuonya wakati hatari inakaribia. Mambo yanapokuwa mabaya, yanapoenda kombo, sikuzote Hiyo itakuwa ni onyo kwako. Halafu basi, badala ya siku moja kuwa kama yule mvulana mdogo tajiri ambaye tunanena habari zake; uwe mtu kama mtume Petro, Paulo, ama mtu aliyewavuta watu kwa Yesu Kristo. Ninyi fanyeni hivyo, enyi watoto.

Twaweza kuomba?

¹¹⁷ Bwana Yesu! Vijana, wanaume na wanawake wa kesho, kama kukiwapo na kesho. Hatuna budi kuwafundisha, Bwana. Tunauhisi mzigo huo, kuwafundisha kana kwamba kutakuwako na kesho. Kama haipo, basi leo hii ndiyo siku.

¹¹⁸ Halafu basi, Baba, tunajua ya kwamba hakuna mtu anayekubalika machoni Pako. Hakuna mwanadamu anayeweza kujitukuza. Hakuna elimu, ingawa vitu hivi vinavyoweza kuwa ni vizuri, hakuna matendo mazuri, hakuna taasisi ya kidini, hakuna saikolojia, hakuna chochote kinachoweza kumthibitisha Mungu ila Roho Mtakatifu. Yeye ndiye Chombo, Mungu Mwenyewe, katika umbo la Uzima wa Milele, kinachoweza kutujia kama mtu binafsi. Nasi tunashukuru kwa ajili ya jambo hili.

¹¹⁹ Hakika limeelezewa wakati Petro alipotoa yale maungamo. Yesu alimwambia, “Mwili na damu havikukufunulia hili. Hukulisoma katika seminari. Hukulisoma katika shule fulani.” Ni jambo la kibinafsi, jambo ambalo kila mtu binafsi hana budi kupokea. Wewe ulisema, “Juu ya mwamba huu nitalijenga

Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayataweza kulishinda.” Tunashukuru kwa ajili ya hilo, Bwana.

¹²⁰ Sauti hiyo ingali hai usiku wa leo. Na kungali kuna vituo, vituo vya mbali, vituo vya kusikilizia, vituo vya kupokea, vya imani, ambavyo vinaweza kulikukubali. Tunaomba ya kwamba kila mmoja wa watoto hawa ataupokea Huo, Bwana, mioyoni mwao. Pia kumbuka ya kwamba, si yale wanayofanya wapate kuwa wema, bali wao. . . Mungu hatuhukumu kwa yale tufanyayo, bali kwa yale ambayo tumekubali. Tunaokolewa kwa imani yetu, na si katika matendo yetu. Kwa hiyo tunaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba hao watapata ono sasa, na kuona na kusikia ule mwaliko mkuu wa Milele, wa “Njoo unifuate.”

¹²¹ Jalia kila mmoja wao, Bwana, ageuke ayaache mambo yote ya ulimwengu, maisha haya yapatikanayo na mauti, yaliyo na mwisho. Kama walivyo hapa usiku wa leo, na nywele zao nyeupe za dhahabu, na wengine wao wakiwa na nywele zao nyeusi, na macho meusi, na macho ya samawati, nao wameketi katika hali yao nzuri kabisa watakayowahi kuwa nayo.

¹²² Na kama vile yule mwandishi mashuhuri alivyosema, “Mkumbuke Muumba wako katika siku za ujana wako, kabla hazijakaribia siku zilizo mbaya. Ndipo hutakuwa na furaha katika hizo.” Jinsi ambavyo, Bwana Yesu, ulimwambia Petro, “Ulipokuwa kijana, uliamka ukaenda ulikotaka. Lakini unapokuwa mzee, mtu mwingine anakupeleka usikotaka kwenda.” Jalia wakumbuke, “Sasa ndiyo siku. Huu ndio wakati.” Tujalie, Baba.

¹²³ Ninamdai kila mmoja wao, kama mwanangu mimi, hapa usiku wa leo, kwa kila mtoto humu ndani. Ninajisikia ya kwamba umeweka mikononi mwangu, kuwalinda. Ninawadai wote, kutoka kwa Shetani na kutoka kwa mauti, waingie Uzamani ndani ya Yesu Kristo. Amina.

¹²⁴ Mbarikiwe, enyi watoto. Ni vema sana kusema maneno machache kwenu. Nami nitarudi tena, Billy. Watoto wazuri, nawathamini. Ndugu Fred, Bwana akubariki. Bwana akubariki, dada.



NJOO, UNIFUATE SWA63-0601

(Come, Follow Me)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumamosi jioni, tarehe 1 Juni, 1963, kwenye Mkutano wa Nyumbani huko Tucson, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku ili yorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org